

The Best Composition KCPE 2003

YALIYOPITA SI NDWELE TUGANGE YATAYO
Siku yenye we ilikuwa ijumaa-Nakumbuka
vizuri sana namna baba alivyopingia nyumbani.
Alikuwa hana furaha hata kidogo. Sote tulikuwa
tumebwakia stafthi yetu bwaku bwaku tayari
kuanza gange ya mchana. Tumwulla baba kitu
kilichomhuzuniha. "Nimetoka shulenii wenu Kulipa karo
na nimepata huko habari ya kusikitisha." Alisema.
"Mwalimu wenu mmoja amedga?" Kusikia hivyo,
tijara niliyokuwa nayo iliniacha na huzuni
ukaniingia. Ilikuwa wazi kwamba Bwana Wemba
ndiye aliyekuwa amepiga dunia teke kuani ni
yeje pekeyake ambaye alikuwa ameugua kwa
muda mrefu.

Mimi nilimpenda sana Bwana Wemba.
alikuwa mwalimu wangu wa hesabu. Yeje alikuwa
na hekima na mawaidha uake ulikuwa mazuri

sana. Mara nydingi - Kabla ya kufunza, Bwana Wemba alituhadithia mifano ya watu ambao hawakuwatii wokuu wa o na mwishowe wakaangamisote tuliyatilia maanani mawaidha uake kwani tulielewa fika kwamba, asiyesikia muonyo ya waku wake husafiria katika mtumbwi wa idonge wa mfinyanzi. Bwana Wemba angefunza nasi tungejiona tukifuzu katika mtihani wa kitaifa. Niliwahurumia wanawe marehemu kwani ulikuwa tu mwezi mmoja uliopita walipomboleza mama yao. Sasa tena walikuwa wamempoteza abu yao. Kwa kweli, zani iliandamaili hiyo kwa mfiuatano wa kutisha. Kwa wanawe Bwana Wembas, yalikuwa baada ya donda msunari ni wa moto.

Shule yetu yote ilihuzuni ka. "Hatutampata mwalimu mwiningine aliye na kipawa kwa hesabu kama Bw. Wembas" wengi walisikika wakisema. Kwa kweli Marehemu mwalimu wetu aliacha pengo kubwa liliokuwa ngumu sana kuziba. Chambilecho wahendaji mkiu ukigwa wana wa ndege huyumba.

Matalayarisho ya mazishi yalipangwa kisha Bwana Wemba akazikwa. Hapo nilitanabahi kwamba maisha ni kama maua yanayonyauka na hatimaye kukauka.

Tuliletewa mwalimu mwiningine wa hesabu. Tulishirikiana pamoja na kutia shime masomoni, kwani, uzi mmoja hauna nguvu, lakini nyuzi nydingi zikisokotwa pamoja hutengeneza kamba madhubuti inayoweza kumfunga ndovu asiweze kujijongeza wala kujifukuta. Tulijifariji kwa kusema kuwa, yalijopita si ndwele tugange yajayo. Tuliendele kutia bidii masomoni ili matokeo yetu

yawe mazuri, kwani tuliiunga mkono methali itetayo, mtaka cha mvunguni ni sharti diname.

Tulifanya mtihani na kuibuka washindi katika tafya zima. Tulijawa na tijara riboribo mithili ya kibyongo aliyedemek samadarini mwake chebichi masi na kupata kuwa ameondokewa na nundu-waama, mchumla juani hulia kivulini.

Mimi binafsi nilifurahi kwani kifo cha bwana Wemba kilikuwa kimezusha hali ya taharuku shulenzi mwetu lakini mwishowe matoked yetu yalikuwa yakupendeza.

(Alama iliyotuzwa 38)

Insha hii ni ya hali ya juu sana na mwandishi ameielewa mada aliyopewa na akaishughulikia viliyvo. Matumizi ya semi, methali na maneno ya msamati hayakupoteza maana anayokusudia katika sentensi zake. Hati yake ni ya kuvutia na kazi yake ameipanga vizuri.

4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

Mwisho, tungependa kupendeleza yafuatayo kwa walimu

1. Funzeni vipengele vyote vya lugha.
2. Wanafunzi ni lazima wafundishwe kuelewa kifungu na kujibu maswali viliyvo.
3. Mfundishe wanafunzi kujibu maswali ya viwango vya juu si tu kuwa wanajua kujibu maswali ya kuhusisha ujuzi peke yake. Ni vizuri wafundishwe kujibu maswali ya tathmini, uchanganuzi nk.
4. Katika uandishi wa insha wanafunzi wafundishwe kufuata mada, kuwa na hati sati, uakifishi ufaao, matumizi ya semi na methali kwa njia inayofaa na kupanga kazi yao vizuri.